

**NENO LA UKARIBISHO LA MHE. ANNA E. MGHWIRA,  
MKUU WA MKOA WA KILIMANJARO WAKATI WA  
UFUNGUZI WA KIKAO CHA KUZUNGUMZIA MIKAKATI  
YA UHIFADHI WA HIFADHI ASILIA YA  
CHOME/SHENGENA TAREHE 16/06/2017**

- Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Moshi na Same;
- Katibu Tawala wa Mkoa;
- Wah. Madiwani;
- Meneja wa TFS Kanda ya Kaskazini;
- Wadau wa Habari;
- Wana Habari;
- Wageni waalikwa;
- Mabibi na Mabwana:

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujalia kukutana hapa siku ya leo.

Aidha napenda kuwashukuru Wakala wa Misititu (TFS) Kanda ya Kaskazini kwa kunialika kuwa Mgeni Rasmi katika shughuli hii.

**Ahsanteni sana!**

**Ndugu Meneja wa Kanda;**

Mkoa wa Kilimanjaro ni miongoni mwa Mikoa ambayo hukumbwa na ukame hususan katika misimu ya kiangazi.

Pamoja na sababu za kidunia miongoni mwa sababu kuu za ukame mkali ni uharibifu wa mazingira hususan uvunaji holela wa bidhaa zitokanazo na misititu.

Hapo awali Mkoa wa Kilimanjaro ulikuwa ni miongoni mwa Mikoa yenye hali ya hewa nzuri iliyokuwa ikiruhusu uzalishaji wenye tija wa mazao ya kilimo.

Lakini hali ilivyo sasa kila mmoja wetu ni shahidi wa hali mbaya ya hewa tunayokabiliana nayo. Kilimo chetu kimekosa uhakika kutokana na mabadiliko ya tabia nchi yaliyotoknaa na uharibifu wa mazingira tulioufanya.

### **Ndugu Meneja Wajumbe;**

Uhifadhi wa maliasili si jukumu la mtu mmoja au kikundi fulani ndani ya jamii. Wakati umefika sasa kwa jamii kuelewa kuwa kila mmoja wetu anawajibu wa kuhakikisha kuwa hifadhi zetu zote zinakuwa salama.

Aidha; Serikali kwa kushirikiana na wananchi pamoja na wadau imekua ikichukua hatua mbalimbali kukabiliana na hali ya uharibifu huo ikewemo kusimamia sheria zinazolinda misitu na hifadhi zote.

### **Ndugu Meneja wa Kanda;**

Sote ni mashahidi kuwa msitu wa Chome ni moja ya hifadhi zinazokabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo **ujangili** wa **uvunaji holela wa miti, uchomaji wa moto** na **shughuli nyingine za kibinadamu.**

Hali hii imepelekea uharibifu mkubwa wa mazingira na kuwepo kwa hatari ya kutoweka kwa hifadhi hii muhimu kwa ustawi wa maisha ya wananchi wetu.

Leo tumekutana hapa ili kuzungumza juu ya uhifadhi wa hifadhi asili ya Chome (Shengena). Napenda kutumia fursa hii kuelekeza mambo yafuatayo:-

- (i) Kila mmoja wetu atoe mawazo yake kwa uhuru na uwazi kwani kukutana kwetu hapa ni ujumbe tosha kuwa mawazo yetu sote yanahitajika na ni muhimu kwa ajili ya maendeleo yam situ huu.
- (ii) Lazima tutambue kuwa tutakachokijadili leo kitatoa mawazo elekezi juu ya kunusuru msitu huu. Hivyo basi; ni matumaini yangu kuwa sote tutatoa mawazo ya kujenga ili tuweze kuyafikia malengo yetu.
- (iii) Vikao hivi viwe endelevu kudumisha umoja, mshikamano na ushirikiano katika masuala ya uhifadhi wa msitu wetu.
- (iv) Wajumbe wote lazima wajikite katika kutafuta ufumbuzi wa tatizo badala ya kulalamika na kulaumu.
- (v) Kila mjumbe afahamu kuwa uhifadhi endelevu wa msitu huu ndiyo siri ya mafanikio ya maendeleo ya wananchi wanaozunguka hifadhi.

Hivyo basi kila mmoja wetu aweke mbele maslahi ya kudumu ya umma atakapokuwa anachangia mawazo yake. Uzoefu unaonesha kuwa kuna baadhi ya viongozi wa kisiasa hudhani kuwarahisishia wananchi mazingira ya kuharibu hifadhi ndiko kuwasadia. Mawazo haya si sahihi kabisa kwani hifadhi hizi tunazilinda kwa maslahi ya wananchi.

## **Ndugu Wajumbe;**

Napenda kuhitimisha kwa kuwashukuru kwa mara nyingine tena Wakala wa Huduma za Mimitu (TFS) Kanda ya Kaskazini kwa kunialika.

Mwisho, napenda kutamka kuwa; **kikao cha kuzungumzia mikakati ya uhifadhi wa hifadhi asilia ya Chome/Shengena kimefunguliwa rasmi.**

**Ahsanteni sana kwa kunisikiliza!**